JUMUIYA YA WANAFUNZI WA ST. JOSEPH, HUU NDIO UMOJA NA MSHIKAMANO WETU. KWA HERI JEMEDARI, KIONGOZI NA RAISI WETU NDUGU BACHUBILA HARUNA

Awali ya yote ningependa tumfahamu mpiganaji, mzalendo na jemedari wa vita dhidi ya mapebali wa kihindi hapa nchini Tanzania ndugu **BACHUBILA HARUNA.** Kama nilivyosema hapo juu huyu ni kiongozi wetu na mpambanaji juu ya haki za wanafunzi na mzalendo kwa taifa lake. Napenda kumpongeza kwa jitihada zake juu ya kupigania madai ya wanafunzi wa mtakatifu yosefu kampasi ya luguruni. Napenda kumpongeza kwa kukumbushia na kuhitaji mrejesho wa WARAKA uliowasilishwa kwa **WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOGIA** wakati wa mgomo. Kiongozi huyu amepigania mambo yafuatayo ndani ya siku 30 za kazi:-

1. Marekebisho ya Canteen
2. kupinga matokeo mabovu na yenye uonevu kwa wanafunzi
3. Ufuatiliaji kulipa ada kwa awamu na kudhamini wanafunzi walioshindwa kulipa ada kwa idadi kubwa

Lakini tumeshindwa kumuonyesha ushirikiano wetu wa dhati baada ya kusimamishwa masomo yake kwa muda wa mwaka mmoja na kupewa masharti magumu ya kurudi chuo. **masharti hayo ni kukanusha barua alizotuma kwenda wizarani (wizara ya Elimu sayansi na teknologia, ofisi ya waziri mkuu na Tume ya vyuo vikuu) na kukanusha kwa maandishi yote ya kwenye waraka yametimizwa chuoni. Ukweli tunaufahamu kuna mambo hayajatimizwa. Akishindwa kufuata hayo maagizo hatoruhusiwa kupewa usaili baada ya kutumikia adhabu hiyo.**

Chakushangaza na kusikitisha baraza lake la mawazir aliowateua kwa kuwaamini ndilo la kwanza kumtelekeza baada ya kupewa hukumu hiyo na kutokuonyesha ushirikiano wowote na kukubaliana na adhabu aliyopewa na uongozi wa chuo, **huu ndio umoja na ushirikiano tuliofundishwa JKT???** Uzalendo ni kutetea maslahi ya watanzania wanyonge na kuliweka Taifa mbele kokote utakakokuwa, tumekubali kumpoteza ndugu yetu, Rais wetu, ndugu

Bachubila Haruna kwa maslahi ya mabepali hawa kutoka india (ukoloni maomboleo). Uko wapi umoja wetu, mshikamano wetu na uzalendo wetu kama wanafunzi na wazalendo wa Taifa letu hili changa? Wako wapi wastaafu wa jeshi waliokuwa na vyeo vikubwa ambao wameajiriwa na mabepali hawa?? Ningependa kuanisha vyeo vyao KANALI Mwaipopo (Second Dean), MEJA Mathew Ngulugulu (chief Dean), MEJA Damas (Assistant lecturer ECE) na LUTENI KANALI Martin Mapujila (assistant registrar), tulitegemea mngeonyesha ushirikiano wenu wa kumtetea Raisi wetu wa chuo kwenye kamati ya maulizo (inquiry committee), Lakini kwa kutetea maslahi ya tumbo lisoshiba na kushindwa kuonyesha uzalendo wa Taifa kama ilivyo mafunzo ya kijeshi. Kwa viapo vya uzalendo mlivyokula jeshini basi nafsi zenu ziwasute.

Kwakutumaini serikali yetu ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania chini ya Rais ndugu DKt. John Pombe Joseph Magufuli na kuiamini, serikali ya wanafunzi imewekwa kwenye taasisi zote za elimu kwa lengo la kuwakuza viongozi wa taifa hili la Tanzania ambao ni wazalendo wa kesho na kesho kutwa watao endeleza gurudumu la uongozi wa Taifa hili na kuyafichua maovu katika taasisi za elimu zilizo rasmi ili kupata wasomi wenye sifa stahiki za kuweza kuzitumia rasilimali za taifa hili la Tanzania.

Kwa haya yote tunaamini serikali yetu tukufu na sikivu ya Tanzania itachukulia uzito swala hili na kuchukua hatua stahiki za kumrudisha masomoni ndugu BACHUBILA HARUNA.

Tungependa wanafunzi wa jumuiya ya mtakatifu yosefu tuutambue uzalendo na mshikamano, hii ndio silaha ya kuokoa taifa letu hili change kutoka kwa mabepali wa kihindi na kupingana na ukoloni maomboleo. Mjitambue kuwa nyie ni wanazuoni na wasomi mnaotegemewa na jamii na taifa kwa ujumla kuleta mabadiliko chanya ndani ya taifa hili.

Mungu ibariki Tanzania

Mungu ibariki st. joseph